

SUALA LA

# Kusaidia Jamii

## Vipi Kitendo Hiki Hujenga Mali za Ndani, Uwezo, Uaminifu—na Kwa Nini ni Muhimu


Kutoka Kenya hadi India hadi Slovakia hadi Brazil, wakazi wameimarisha shule, wametengeneza ajira, raia wamepewa uwezo, wameimarisha mashirika, na kuhamasisha wafadhili.

Vipi jamii hizi zilifanya?

**Zilijigeuza kuwa jamii za kusaidia**

# Matendo ya Ndani, Kusambaa Kidunia

**Katika Slovakia**, Taasisi ya Mji wa Banská Bystrica ni taasisi jamii ya kwanza Ulaya Mashariki. Ingawa ilianza kupitia mradi wa Afya wa Miji wa Shirika la Afya Duniani, sasa ina mkusanyiko wa wafadhili wa ndani na imebadilisha mikakati yake kuwa ya ubunifu wa raia wenyewe. Taasisi husaidia vikundi vinavyosaidia watoto wa mitaani wa mji, imesaidia kuunda shirika linalosaidia jamii ya ndani ya Roma, huendesha Benki ya Vijana ili kuwashirikisha vijana wakazi katika kutoa misaada,na—katika kile mkurugenzi mtendaji wake, Beata Hirt, kipindi aliyaita mafanikio makubwa—"imeonyesha kwa raia wa ndani kwamba wana nguvu  na uwezo wa kutosha  kutatua matatizo yao wao wenyewe."



**Katika Brazil**, chuo cha Comunitário Grande Florianópolis, au ICom, kiliundwa na wanaharakati wa ndani kuimarisha mashirika dhaifu ya kijamii. Kazi ya ICom inavutia kwa sababu nyingi. Huwahamasisha wafadhili wa ndani kuwekeza katika maendeleo ya jamii. Huainisha mali za jamii na kuonyesha mambo ya ndani. Wanaendeleza ubunifu wa matumizi ya teknolojia jili ya manufaa ya kijamii. Na wanafanya fikra za taasisi jamii kufanya kazi katika Brazil. "Tumejifunza kuwa tunahitajika kwanza kushawishi utamaduni wa utoaji wa mpangilio," alisema Anderson Giovani da Silva, Mkurugenzi Mtendaji wa ICom. "Halafu tutoe nyenzo kusaidia mashirika ya kijamii, wafadhili binafsi, kampuni na serikali kufanya kazi pamoja."

**Katika Kenya**, shirika linaloitwa Ushirika wa Maendeleo ya Jamii Makutano (UMAJAMA) lina orodha ndefu ya mafanikio, ikiwa ni pamoja na kujenga mabwawa manne na visima 17 na kuendeleza ekari 10,000 za ardhi yenye rutuba Wakati matokeo haya yanavutia, kinachoonekana kuhusu habari hii ni jinsi shirika lilivyojenga uwezo wa wakazi kutawala maendeleo yao wenyewe. Rafaeli Masika, kiongozi wa eneo aliyekuwa kinara katika kuunda UMAJAMA anaelezea ahadi ya shirika kujengea jamii uwezo wa muda mrefu kama hivi: "Watu katika Kenya sio maskini kwa sababu ya kukosa rasilimali, bali kwa sababu wanakosa uelewa wa namna ya kutumia rasilimali."

**Katika India**, zaidi ya wakazi 5,000 kupitia vijiji 50 waliungana pamoja kama wanachama wa Taasisi ya Prayatna. Chini ya kanuni ya "Utatuzi wa ndani wa matatizo ya ndani," waliwahamasisha wakazi, Daliti na Waislamu zaidi, kuchangia muda wao, chakula, fedha, na rasilimali zingine kuelezea haki za binadamu kwa ufanisi, makazi, ajira, uwajibikaji wa serikali, na haki za kijamii. Shirika limeendeleza ujuzi wa viongozi wa ndani, kujenga mahusiano mazuri kati ya jamii za Wahindu, na Waislamu, na kuendeleza nguvu za utendaji wa pamoja. "Wakati tunapoenda wenyewe, hawatusikilizi," alisema mjumbe mmoja, "lakini mara zote tunasikilizwa tunapoenda pamoja."


Kwa taarifa zaidi za ufafanuzi wa Kenya, na nyingine nyingi, tafadhali tembelea Mfuko wa Taasisi za Jamii katika www.globalfundcommunityfoundations.org.

# Ufumbuzi katika Kupanda

Kote duniani, raia huleta vitendo vya kusaidia jamii[1] katika maisha kwa namna ya kila mabadiliko. Wanaunda na kuendesha taasisi mpya ambazo zinaibuka na kutoa fedha za ndani na mali zingine. Wanarekebisha mipango kukidhi mahitaji ya jamii na kuongeza ufahamu juu ya mambo ya ndani. Wanakutanisha viongozi wa kijamii, kuimarisha jumuiya za kiraia, na kupanga kwa muda mrefu.

Mashirika ya hisani jamii yanaongezeka. Kati ya mwaka 2000 na 2010, aina moja—taasisi jamii—zilikua kwa kiwango cha 86%, ikiwa na wastani wa kuundwa taasisi 70 kila mwaka.[2] Sababu kadhaa zimeonyeshwa kuelezea ukuaji huu, ikiwa ni pamoja na mashirika yanayosaidia maendeleo ya haya matendo, mfumo wenye nafasi ya kubadilika, utoaji fedha wa muda mrefu na upanuzi wa juhudi za kujenga jumuiya za kiraia kote duniani.

IDADI YA TAASISI JAMIIS 2000-2010




Wakati taasisi jamii ndio muundo maarufu zaidi wa kusaidia jamii,aina mpya za mashirika yanapanua wigo wa vitendo. “Kwa miaka mingi iliyopita, kumekuwa na wimbi jipya la mashirika ya kusaidia jamii,” anasema Halima Mahomed wa TrustAfrika. “Yako hai, hutokana na muktadha wenyewe, hayatawaliwi na jambo fulani, na hayaingilii mitizamo ya wahisani jamii wengine.”

Kwa kiini chake, kusaidia jamii huanzia kwa mtu wa ndani kumsaidia mwingine, mali itokeayo yenyewe hupatikana katika jumuiya na desturi zote. Kiukweli, watendaji wengi hufananisha kitendo hiki na msisimko wa jamii na zaidi kama muundo wa shirika.

Kutokana na kwamba hisani jamii kipekee huweza kupitisha msisimko huo hadi taasisi za mwisho za ndani, na zina nafasi ya kubadilika kuwa hali halisi ya ndani na kuwa wafadhili wa ndani, hakuna shaka kwamba jamii zinapata shauku.

> “Kumekuwa na mabadiliko juu ya namna hisani jamii zinavyotekelezwa katika mataifa yanayoendelea. Imeondolewa kutoka nia kubwa ya Marekani Kaskazini kwenye mahitaji ya wafadhili na inabadilika zaidi. Ubunifu unatoka Afrika, Asia, na Latini Amerika.”
>
> **AVILA KILMURRAY, TAASISI JAMII YA IRELAND KASKAZINI**

[1] *Kama ilivyofafanuliwa katika Thamani ya Kusaidia Jamii*, mfululizo wa majadiliano ya mwaka 2010-2011 kati ya wahusika na wafadhili yalijenga “tafsiri kwa tabia” ya hisani jamii, pamoja ile “ya kupangwa na kuumbwa,” “iinajielekeza yenyewe,” “hufanya kazi kama mjenzi aliyefunguka,” “hujenga jumuiya za kiraia,” “hutumia mali na fedha za ndani,” na “hutafuta kushirikisha watu wote na jamii ya u sawa.” Taarifa ilizinduliwa na, Taasisi ya Aga Khan Marekani na Taasisi ya Charles Stewart Mott na kutayarishwa na Barry Knight, Inapatikana katika http://www.mott.org/files/publications/thevalueofcommunityphilanthropy.pdf.

[2] *Ona taarifa ya mwaka 2010 ya Nafasi ya Taasisi Jamii*, iliyoandaliwa na Juhudi za Dunia za Kusaidia Watoa Ruzuku (JUDUKUWARU).

# Mantiki ya Kusaidia Jamii

Kwa sehemu jamii zinageukia kwenye hisani jamii kwa sababu vitendo hivi hupelekea matokeo mazuri ya maendeleo. Kutokana na Jenny Hodgson wa Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii, kuna mantiki yenye nguvu katika kusaidia jamii, nyingi ya fikra ni kama juu ya namna itakavyoweza kutengeneza matokeo ya muhimu kwa wakazi, wafadhili, na watendaji:

- Kama watu watajiona kuwa sehemu ya wawekezaji katika maendeleo yao wenyewe, hivyo watajali zaidi juu ya matokeo.
- Kama wakazi huleta mali zao wenyewe katika meza, hivyo nguvu ya mabadiliko huwa sawa ili kwamba ni ubia, siyo uhusiano wa kawaida wa mfadhili—mnufaikaji.
- Kama watu wa ndani wanamiliki na wanatoa kusaidia jamii, hivyo wapokeaji wa ndani wanakuwa wawajibikaji katika namna ambayo hujenga mtaji wa jamii
- Kama taasisi za kusaidia jamii zinaweza kuwa kama mahali pa kuhifadhi aina mbalimbali za fedha na mali, hivyo wanaweza kuendesha maendeleo kwa njia ya mafanikio.

Watendaji na wasaidia hisani jamii wametambua sehemu tatu  kuu zinazojenga jambo hili:

**MALI**

Kusaidia jamii kujenga na kutumia mali za ndani—fedha na vinginevyo. Hii ndiyo sababu wafadhili binafsi na taasisi za wafadhili hufikiria kama njia sahihi kwa uendelevu, ukuaji wa msingi wa raslimali kwa kazi katika maswala ya jamii. Matumizi ya mali za ndani, ushirikishwaji wa wafadhili wa ndani, na matumizi ya mara kwa mara ya utoaji wa fedha vyote vinaruhusu hisani jamii kuimarisha jumuiya za kiraia kwa muda mrefu ujao.


**UWEZO**

Mashirika ya hisani jamii hujenga uwezo wa muda mrefu katika namna ya mahusiano, ufahamu, miundombinu, na uongozi muhimu kwa jumuiya za kiraia—uwezo ambao mifumo ya muda—mfupi haiwezi kuendeleza. Kiuhalisia, hisani jamii ni njia inayofaa  kuimarisha sauti na ushiriki wa wakazi. Na imewekwa—vizuri kusaidia mashirika kupokea hali ya mabadiliko, vipaumbele vipya vya ndani, mabadiliko ya nia za wafadhaili, na fursa za uongozi.

**UAMINIFU**

Kupitia ukuaji wa uongozi wa ndani na maamuzi ya wazi ya ufadhili, hisani jamii hujenga uaminifu wa wakazi katika taasisi zao za ndani na kila mwingine. Huu mtaji wa kijamii huimarisha jumuiya za kiraia. Huchochea ushiriki. Hujenga hisia za umiliki wa ndani wa mchakato wa maendeleo. Na hufanya mashirika ya hisani jamii kukusanyika kwa ufanisi, kuarifu,na kuhamasisha wakazi kwa namna ambayo mashirika mengine mara zote hayawezi.

# Njia ya Matokeo Mazuri



# Mwito kwa Vitendo

Idadi kubwa ya wafadhili, watendaji, na washawishi wameanza kuangalia namna ya kuimarisha na kukuza taasisi jamii kidunia kama mkakati wa maendeleo, vitendo vya hisani, na nguvu ya jamii.

Kufikia kilele chake na kuleta matokeo kama vitendo vya ufanisi vya maendelo, hisani jamii zinahitaji msaada. Msaada kama huu lazima utegemee mahitaji ya jamii, ikiwa na umakini wa kuzingatia nini kinafanyika katika eneo, na isilazimishwe na ajenda za nje. Mwito wa msaada unaungwa mkono na utafiti. Kwa mfano, JUDUKUWARU 2010 *taarifa ya nafasi ya Taasisi Jamii Duniani*, walikuta kwamba ubashiri mzuri wa ukuaji mpya katika taasisi jamii kati ya mwaka 2008 na 2010 ilikuwa ni uwepo wa mashirika ya kitaifa au kimkoa yaliyosaidia maendeleo ya taasisi hizi mapema katika muongo.

Na inasaidiwa na hisia za fursa. Taasisi jamii zimethibitisha kuwa na ufanisi na kufaa katika aina za muktadha wa kijiografia na kimila. Ni muda muafaka kuzisaidia kuwa njia ya mikakati ya maendeleo. Kwa teknolojia ilivyofanya kuwa rahisi kwa wafadhili wa nje kutoa fedha kwa jamii zilizo mbali, mashirika ya misaada ya ndani yanatakiwa kuweka vizuri na kutawala uwekezaji huu. Kwa matendo haya kuendelea kuimarika na kukua, sasa ni muda wa kuchukua hatua.

"Tumefanya kazi katika jumuiya za kiraia kwa muda mrefu. Wakati watu kwa wenyewe wanapofanya vitu, programu hizi huwa **ENDELEVU** zaidi. Uongozi, rasilimali, fedha, na msaada wa hiari vyote vinaendelezwa"

**MIRZA JAHANI, TAASISI YA AGA KHAN**

"Katika baadhi ya maeneo, njia pekee ya kuwa na ufumbuzi utakaofanya kazi ni kwa njia ya watu kuja **PAMOJA** wenyewe. Tunataka namna ambayo jamii zinaweza kusukumwa na kuletwa pamoja"

**TADE AKIN AINA, KAMPUNI YA CARNEGIE**

"Tunakwenda ndani katika mabega ya watu ambao **JAMII** inawafahamu na kuwaamini"

**FELECIA JONES, TAASISI JAMII YA BLACK BELT**

"Hatua kwa hatua tunakuwa chanzo cha taarifa na **ELIMU JUU YA JAMII**."

**LÚCIA DELLAGNELO, INSTITUTO COMUNITÁRIO GRANDE FLORIANÓPOLIS**

"Tulitaka **KUBADILISHA** jamii kutoka ndani."

**MARWA EL DALY, TAASISI YA WAQFEYAT AL MAADI**

# Vipi Tunaweza Kusaidia Vitendo Hivi Kustawi?

Washawishi wanagundua maswali mengi wanapotengeneza mikakati kukuza eneo hili:

- Vipi tunaweza kutoa fursa zaidi za mtandao wa rika—kwa—rika na kubadilishana uelewa kati ya watendaji wa hisani jamii?
- Vipi tunaweza kuendeleza uelewa wa hili suala kupitia tafiti, tathmini, na mawasiliano?
- Zipi ni njia sahihi za kusaidia mashirika ya hisani jamii yanayojitokeza kuwa na msimamo?
- Namna gani wafadhili wa nje wanaweza kusaidia hisani jamii huku wakipunguza mabadiliko ya "kutoka—nje" ambayo yanaweza kuzuia bidii kama hizi?
- Aina gani ya miundombinu ya kimataifa ingeweza kufadhili majaribio, kutengeneza nyenzo, kuchangisha fedha, kuainisha mali, kukutanisha viongozi, kuunda mitandao, na kuimarisha vitendo?
- Vipi tunaweza kujenga harakati za taasisi jamii kidunia?

"Hisani jamii hutoa nafasi kwa majribio. Tu wadogo lakini **TUNABADILIKA** Tunaweza kuziba mapengo. Ni juu ya majaribio na kuwa mjasiriamali."

**JAN DESPIEGELAERE, TAASISI JAMII FLANDERS–MAGHARIBI**

"Ni changamoto kwa wafadhili wa nje wanaowekeza kiasi kikubwa cha fedha kutegemea programu kuendelezwa. Kutokana na uzoefu wetu, kazi huendelea pale unapokuwa na hisani jamii inayosaidiwa. **INAFANYA KAZI**."

**SHANNON LAWDER, C.S. TAASISI YA MOTT**

"Kupitia hisani jamii, **WADAU WA NDANI** wanaweza kumiliki wenywe maendeleo yao."

**MARYANNE YERKES, AJENTI WA MAENDELEO YA KIMATAIFA MAREKANI**

"Tulikuwa tunabishana kwamba (kujenga) tu kisima haitoshi, kwa sababu hayo siyo maendeleo. **MAENDELEO**, tuliyokuwa tukibishania, ni habari juu ya kisima....Ulijenga uwezo wa ndani? Ulibadilisha tabia? Ulisaidia jamii kufikiria tofauti?"

**MONICA MUTUKU, ZAMANI, WA TAASISI YA MAENDELEO KENYA**

# Jiunge na Kazi!

Mashirika mengi yameungana kuzindua muungano wa wasaidia taasisi jamii kujibu maswali haya na kuimarisha eneo hili. Wanakukaribisha kujiunga nao.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Jenny Hodgson
jenny@globalfundcf.org
www.globalfundcommunityfoundations.org

Imetafsiriwa na:

Elikira Kweka, D.
Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto,
Idara ya Kilimo, Mifugo na Ushirika,
S.L.P 22, Lushoto,
Tanzania.
Simu: 255753108549/255787043746
Barua pepe: elkweka2013@gmail.com

**TAASISI YA AGA KHAN MAREKANI**
1825 K Street NW, Suite 901
Washington, D.C. 20006
www.akdn.org
info.akfusa@akdn.org
+1.202.293.2537

**TAASISI YA CHARLES STEWART MOTT**
Mott Foundation Building
503 S. Saginaw Street, Suite 1200
Flint, MI 48502
www.mott.org info@mott.org
+1.810.238.5651

**MFUKO WA DUNIA WA TAASISI JAMII**
Fourth Floor, 158 Jan Smuts Avenue Rosebank
Johannesburg 2196 South Africa
www.globalfundcommunityfoundations.org
info@globalfundcf.org
+27.11.447.4396

**MFUKO WA NDUGU WA ROCKFELER**
475 Riverside Drive, Suite 900
New York, NY 10115
www.rbf.org
communications@rbf.org
+1.212.812.4200

Picha: © Taasisi ya Aga Khan (Jean-Luc Ray, Zahur Ramji), Taasisi ya C.S. Mott, Mfuko wa Dunia wa Maendeleo ya Taasisi Jamii, Washiriki Sedway / Ubunifu: Bluesoup